



Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI



# YALIYOMO

04 Utangulizi

05 Elimu kwa umma

09 Kaguzi mbalimbali

11 Uteketezaji wa bidhaa

13 Habari picha

## BODI YA UHARIRI

■ **Mhariri:**  
Anitha Mshighati

■ **Mwandishi:**  
Maria Sanga





# MAELEZO YA MENEJA WA KANDA



**Bi. Anitha Mshighati**  
Kaimu Meneja wa TMDA  
Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

**N**inayo heshima na furaha kubwa kuwasilisha na kuleta kwenu jarida la kwanza la matukio mbalimbali yaliyojitokeza ndani ya Kanda ya Nyanda za juu kusini katika kipindi cha miezi sita (6) ya kuanzia Julai hadi Disemba, 2021.

Jarida hili limeeleza matukio mbalimbali ya shughuli zilizotekelezwa katika Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Kanda ya Nyanda za Juu Kusini katika kutimiza lengo la kulinda afya ya jamii kwa kusimamia usalama, ubora na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

**Katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2021 Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilitekeleza kazi zifuatazo: -**

- i. Kukagua maeneo mbalimbali yanayotoa huduma za dawa, vifaa tiba na vitendanishi kama hospitali, vituo vya afya zahanati, famasi, maduka ya dawa muhimu za binadamu na mifugo na maabara.
- ii. Kusimamia uteketezaji wa dawa na vifaa tiba vilivyokutwa kinyume na sheria na vilivyoisha muda wake wa matumizi.
- iii. Kusajili na kutoa vibali vya biashara za dawa, vifaa tiba na vitendanishi.
- iv. Uhamasishaji wa wataalamu wa afya katika vituo vya kutolea huduma za afya juu ya utoaji wa taarifa za madhara ya dawa.
- v. Kanda ilitoa elimu kwa jamii juu ya bidhaa za dawa, vifaa tiba, vitendanishi pamoja na tumbaku, elimu hii ilitolewa kupitia vyombo vya habari, vikao na mikutano.

Hivyo basi, nachukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza watumishi wa TMDA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa kutekeleza majukumu ya msingi ya kulinda afya ya jamii kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Disemba, 2021 pamoja na wadau wetu wote kwa ushirikiano wao waliotupa.

# UTANGULIZI

**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)** ) ni Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Afya. Taasisi hii ina jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ni miongoni mwa Ofisi nane (8) za kanda za TMDA nchini. Kanda hii ilianzishwa mwaka 2007 na inasimamia udhibiti katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Rukwa, Iringa na Songwe. Mwaka 2021 Julai mkoa wa Iringa ulikabidhiwa Kanda ya Kati.

Majukumu yanayoratibiwa na Ofisi ya Kanda ni pamoja na kufanya usajili wa majengo yanayozalisha, kuhifadhi na kuuza bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi; kufanya ukaguzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika soko; kukusanya sampuli za dawa, vifaa tiba na vitendanishi kwa ajili ya uchunguzi wa kimaabara; kudhibiti uingizaji nchini na usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi; kutoa elimu kwa umma juu ya bidhaa zinazodhibitiwa pamoja na matumizi sahihi ya bidhaa hizo.

Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inawakaguzi wake katika vituo vya forodha vya Kasumulu na Tunduma ambao jukumu lao kuu ni kuhakikisha kwamba dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyoingia na kutoka nchini vinafuata sheria ya Dawa na Vifaa Tiba sura 2019.





# ELIMU KWA UMMA

## ELIMU YA ATHARI ZA TUMBAKU

Mnamo mwezi Disemba 2021, timu ya wataalamu kutoka TMDA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walitoa elimu juu ya athari za matumizi ya tumbaku kwa makundi mbalimbali ya jamii katika Mkoa wa Rukwa.



Elimu hiyo ilitolewa wakati wa zoezi la utoaji wa elimu kwa umma juu ya majukumu ya TMDA na jukumu jipya la udhibiti wa bidhaa za Tumbaku lililofanyika kwa makundi mbalimbali ya wadau wakiwemo viongozi wa kamati za maendeleo za Kata, Wananchi pamoja na wanafunzi wa vyuo vya Uganga na Uuguzi.

Zoezi hilo lilifanyika mwezi Disemba, 2021 katika kata za Muse, Mpwapwa, Ikozi na Mwadui zikienda sambamba na wananchi katika vijiji vya Mtakuja, Isasa, Kamuhando, Chonga, Kaliko, Katete, Mtuntumbe pamoja na Sopa wakati vyuo vilivyo fikiwa ni vyuo vya St. Bakhita na Sumbawanga Training College.





Katika kuhakikisha kuwa elimu hiyo inawafikia watu wengi zaidi TMDA ilitumia pia vyombo vya habari ikiwemo vituo vya redio vya Nkasi FM, Chemchem FM na Ndingala FM vyote vya Mkoani Rukwa.

Lengo la elimu hiyo ni kuelimisha umma juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa za Tumbaku, pamoja na kueleza juu ya mikakati mbalimbali iliyowekwa ya kudhibiti matumizi holela ya tumbaku ili kuwalinda wasio tumia na watoto walio na umri chini ya miaka 18 kama ambavyo jukumu kubwa la TMDA ni kulinda afya ya Jamii.



Kwa mujibu wa tafiti zilizofanywa na Shirika la Afya Dunia ni (WHO) juu ya athari za moshi wa sigara na bidhaa zingine za tumbaku, takribani watu milioni nane (8,000,000) hufariki duniani kila mwaka kutokana na matumizi ya tumbaku ambapo kati yake vifo milioni moja na laki mbili (1,200,000) vinatokana na kuvuta moshi kutoka kwa mtumiaji aliyekaribu (Passive smoking).



Kutokana na hayo Wizara ya Afya, mnamo Aprili, 2021 ilikabidhi rasmi jukumu la udhibiti wa bidhaa za tumbaku kwa TMDA baada ya kusainiwa kwa kanuni za udhibiti wa bidhaa za Tumbaku chini ya kifungu namba 18 sura ya 121 ya sheria ya udhibiti wa bidhaa za Tumbaku ya mwaka 2021.

## SIKU YA UKIMWI DUNIANI

TMDA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilishiriki maonesho na maadhimisho ya siku ya UKIMWI Duniani yaliyofanyika kitaifa mkoani Mbeya kuanzia tarehe 24/11/2021 hadi tarehe 02/12/2021 ambapo kilele chake kilikuwa tarehe 01/12/2021 katika viwanja vya CCM - Ruanda Nzovwe katika Jiji la Mbeya.



Lengo la TMDA kushiriki maadhimisho na maonesho hayo ni kutoa elimu kwa jamii juu ya kazi mbalimbali za TMDA zinazochangia katika vita vya kupambana na ugonjwa wa Ukimwi ikiwa ni pamoja na kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo.



Katika mwaka 2021 TMDA imesajili jumla ya aina za dawa 15 za kufubaza makali ya virusi vya Ukimwi, dawa 6 za kuzuia magonjwa nyemelezi, ambapo zaidi ya watu 360 walitembelea banda la TMDA na kupata elimu hiyo.





Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. (MB) Kassim Majaliwa Majaliwa ndiye aliyekuwa mgeni rasmi katika kilele cha maadhimisho hayo yaliyokuwa na kauli mbiu ya 'Zingatia Usawa, Tokomeza UKIMWI, Tokomeza Magonjwa ya Mlipuko'.





# UKAGUZI WA DAWA NA VIFAA TIBA

## UKAGUZI WA KIWANDA CHA DAWA NA VIFAA TIBA CHA MSD-IDOFI

Timu ya wataalamu kutoka TMDA Makao Makuu kwa kushirikiana na Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilitembelea na kukagua kiwanda cha dawa na vifaa tiba kinachojengwa na Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Makambako Mkoa wa Njombe mwezi Novemba 2021.



Lengo la ukaguzi huo lilikua ni kujua hatua ambazo mradi wa kiwanda umefikia pamoja na kuhakikisha kuwa ujenzi unazingatia ushauri wa kitaalamu.





Katika ziara hiyo jopo la wataalamu kutoka Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba liliwataka wasimamizi wa ujenzi wa kiwanda hicho kuhakikisha wanazifuata kanuni za uzalishaji bora kwa kuandaa nyaraka zote muhimu za uendeshaji.



Mradi wa ujenzi wa kiwanda cha Dawa na Vifaa Tiba wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD) wa Idofi unatarajia kuzalisha gloves 20,000 kwa saa.



Kadhalika, kiwanda kitazalisha dawa mbalimbali aina ya Paracetamol, Amoxicillin, Arythromycin, Ampiclox kwa uwezo wa kuzalisha Vidonge 330,000 hadi 425,000 kwa saa. Aidha Kiwanda cha dawa za maji kitazalisha jumla ya chupa 180 kwa saa na dawa hizi ni pamoja na Cough Syrup, Paracetamol Syrup, Cotrimoxazole Syrup na Metronidazole syrup.



## UKAGUZI WA HOSPITALI ZINAZOZALISHA MAJI NA GESI TIBA

Wamiliki wa hospitali zinazotengeneza maji na gesi tiba Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wametakiwa kuhakikisha wanazalisha bidhaa zenye ubora, usalama na ufanisi ili kuendelea kulinda na kuimarisha afya ya jamii.

Kauli hiyo ilitolewa na timu ya wataalamu wa TMDA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakati wa ziara ya kukagua hospitali zinazozalisha maji na gesi tiba. Lengo la ukaguzi huo ulikua ni kuangalia wazalishaji kama wanafuata kanuni za uzalishaji bora wa bidhaa hizo.



Mambo yaliyoshauriwa na timu hiyo ni pamoja na kuweka mifumo ya kupima ubora wa bidhaa inayozalishwa, kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wataalamu na kuajiri watumishi wenye taaluma, kuongeza ukubwa wa vyumba vya kuzalishia na kutunzia, kufanya matengenezo ya mashine mara kwa mara na kuweka mifumo ya usimamizi bora.

Hospitali zilizotembelewa ni pamoja na hospitali ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Consolata (Ikonda), Mbozi Mission, Igogwe, Ilembula na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mbeya zilizopo mkoa wa Songwe, Mbeya na Njombe.



# UTEKETEZAJI NA KUKABIDHI BIDHAA

## UTEKETEZAJI

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilitoketeza bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora na usalama zenye uzito wa tani 0.7375 zenye thamani ya shilingi 22,557,975. Dawa zilizotoketezwa ni zile zilizokamatwa baada ya kukutwa na makosa mbalimbali katika kaguzi zilizofanyika katika kipindi cha mwezi cha miezi sita Julai-Disemba, 2021 na Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.



Timu ya wakaguzi wa dawa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakiteketeza dawa na vifaa tiba visizokuwa na ubora na usalama vilizokamatwa kwenye kaguzi maalumu.

Dawa zilizotoketezwa zilikutwa na makosa ya kuisha muda wa matumizi, kutokusajiliwa pamoja na dawa duni.

Zoezi hilo la uteketezaji wa bidhaa za dawa na vifaa tiba umejumuisha dawa ambazo zilikamatwa katika kaguzi na zile ambazo wamiliki wa maduka walileta maombi ya kutoketezwa.

Wito ulitolewa kwa wauzaji na wamiliki wa maduka muhimu ya dawa kuzingatia Sheria na kuacha kutanguliza masilahi yao mbele.



## KUKABIDHI BIDHAA ZA DAWA

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini ilikabidhi dawa zenye thamani ya shilingi 20,859,400, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Dawa zilizokabidhiwa ni zile zilizokamatwa zikiuzwa kimakosa kwenye maduka ya dawa muhimu (DLDM) zikiwa katika hali nzuri ya matumizi wakati wa kaguzi mbalimbali zilizofanyika katika mikoa ya Mbeya na Songwe katika kipindi cha Julai hadi Disemba, 2021.

Mgawanyo wa dawa hizi ulikuwa ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Songwe wamepokea dawa zenye thamani ya shilingi 11,359,400/= na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ikiwa ni shilingi 9,500,000.



Mkaguzi wa dawa msaidizi Kanda ya Nyanda ya Juu Kusini **Bw. Selemani Mayala** akimkabidhi dawa mganga mkuu wa halmashauri ya wilaya ya Mbeya, **Dkt. Yahaya Msuya**

Akipokea dawa hizo kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya Dr. Yahaya Msuya aliipongeza Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kwa kazi kubwa ya kudhibiti bidhaa za dawa vifaa tiba na vitendanishi ilivyosaidia kukamatwa kwa dawa hizo.

Dr. Msuya aliiomba TMDA kuongeza nguvu katika kuimarisha kaguzi kwenye vituo binafsi vya kutolea huduma za afya, hasa maduka ya dawa muhimu kwani kwa sasa ndio kimbilio la kwanza la jamii kupata huduma.

Pia aliongeza kuwa anaiomba TMDA iongeze kiwango cha faini kitakachosababisha watu wasirudie kufanya makosa kwa kuwa kiwango kinachotozwa kinasababisha watu warudie makosa wakijua watamudu kulipa.



Mkaguzi wa dawa msaidizi Kanda ya Nyanda ya Juu Kusini **Bw. Jeffrey Kikoti** akimkabidhi dawa Kaimu mganga mkuu wa mkoa wa songwe, **Bw. Sdney Mdoe**.

Naye Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Songwe Sdney Mdoe aliishukuru (TMDA) kwa kuwakumbuka katika mgao wa dawa hizo zitakazosaidia katika vituo vya kutolea huduma za afya vilivyo mkoani Songwe.



# HABARI PICHA

## MATUKIO KATIKA PICHA KUENZIA JULAI -DISEMBA 2021



Kaimu Meneja wa Kanda Nyanda za Juu kusini Bi. Anitha Mshighati akiwa katika zoezi la ukaguzi wa maduka ya dawa katika mkoa wa Songwe



Mkaguzi wa dawa Msaidizi Kanda Nyanda za Juu kusini Bw. Jeofrey Kikoti akiwa katika zoezi la ukaguzi wa maduka ya dawa katika mkoa wa Rukwa



Mkaguzi wa dawa Msaidizi Kanda Nyanda za Juu kusini Bw. Jeofrey Kikoti akiwa katika zoezi la ukaguzi wa maduka ya dawa katika mkoa wa Mbeya.



Mkaguzi wa dawa Kanda Nyanda za Juu kusini Grace Kapande akitoa elimu ya matumizi ya dawa kwa wanafunzi wa sekondari ya Sumagha iliyopo Mkoa wa Songwe



Kaimu Meneja wa Kanda Nyanda za Juu Kusini Bi. Anitha Mshighati akitoa elimu ya madhara ya tumbaku kwa wananchi wa kata ya Kilando kijiji cha Mtakuja Mkoani Rukwa.



Ndugu. Asifiwe Mboneke mwanachi wa mkoa wa Rukwa akiuliza swali baada ya kupewa elimu juu ya athari za matumizi ya tumbaku.





Kaimu Meneja wa Kanda ya Nyanda za Juu kusini Bi. Anitha Mshighati akitoa elimu juu ya majukumu ya TMDA na udhibiti mpya wa bidhaa za Tumbaku kwa wajumbe wa Kamati ya Maendeleo katika kata ya Mpwapwa Mkoani Rukwa



Mkaguzi wa dawa Kanda Nyanda za Juu kusini Dkt. Sylvester Mwidunda akiwa katika zoezi la utoaji elimu juu ya matumizi ya dawa katika shule ya sekondari Iponjola katika Halmashauri ya wilaya ya Rungwe.



Afisa Elimu kwa Umma Bw. James Ndege akiwa katika zoezi la utoaji elimu ya majukumu ya TMDA kwa wanafunzi wa shule ya Sekondari ya Lupoto katika Halmashauri ya wilaya ya Rungwe.



Mwalimu Nelson Jaston wa shule ya Sekondari Rsushoto akito shukrani kwa TMDA baada ya kupata elimu ya majukumu ya TMDA.



Kaimu Meneja wa Kanda Nyanda za Juu kusini Bi. Anitha Mshighati akipata maelezo ya namna ya uzalishaji wa maji tiba katika Hospitali ya Igogwe wilayani Rungwe,



Timu ya wataalamu ya wakaguzi wa dawa toka makao makuu na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakimsikiliza Mfamasia wa bohari ya dawa Bw. Ezekiel Gadau





Afisa uhusiano Prisca Matagi akitoa elimu ya majukumu ya TMDA kwa wanafunzi wa Chuo cha St. Bakhita cha Nkasi - Rukwa



Kaimu Meneja wa Kanda Nyanda za Juu kusini Bi. Anitha Mshighati akimkabidhi nyaraka za TMDA Katibu Tawala mkoa wa Songwe Bw. Misaile Musa.



Kaimu Meneja wa Kanda Nyanda za Juu Kusini Bi. Anitha Mshighati akitoa maelekezo kwa wakaguzi ngazi ya Mkoa na Halmashauri katika Mkoa wa Njombe.



Afisa elimu kwa umma TMDA Kanda Nyanda za Juu Kusini Bi. Maria Sanga akitoa elimu ya matumizi sahihi ya dawa kwa wageni waliotembelea banda la TMDA katika maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani.



Watumishi wa TMDA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakimsikiliza Mkurugenzi Mkuu Bw. Adam Mitangu Fimbo kwenye mkutano wa mtandao aliyekuwa akihutubia watumishi wa TMDA.



Timu ya wakaguzi wa dawa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini wakitekeza dawa zisizokuwa na ubora na usalama zilizokamatwa kwenye kaguzi maalum ya Mkoa wa Songwe.





Tanzania Medicines & Medical Devices Authority



**MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA**  
**Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**  
**Jengo la Bima ya Afya**  
**Ghorofa ya 3**  
**S.L.P 6171, Mbeya**  
**Simu: +255 25 250 4425**  
**Barua Pepe: [info.mbeya@tmda.go.tz](mailto:info.mbeya@tmda.go.tz)**